# UCHUMI & BIASHARA u&b

## Wafanyabiashara wataka uwazi katika kodi

Na Hyasinta Timothy

ASILIMIA kubwa ya wafanyabiashara wa utalii nchini wapo tayari kulipa kodi kama serikali itaweka utaratibu na mfumo wa wazi utakaoonesha jinsi fedha hizo zinavyotumika kwa ajili ya manufaa ya taifa nzima.

Hayo yamo katika uchambuzi wa ripoti ya nne ya kila mwaka ya mtazamo wa viongozi wa biashara nchini Tanzania ambayo inatoa muhtasari wa mitazamo yao kuhusu mazingira wezeshi na nafasi ya serikali katika kuhakikisha biashara inafanywa kwa urahisi.

Ripoti hiyo imeratibiwa na BEST-AC, taasisi ambayo husaidia Jumuiya za Sekta Binafsi (PSOs) kushiriki katika mazungumzo kati ya sekta binafsi na ya umma kwa lengo la kushawishi mabadiliko kwenye sera za umma za kuboresha mazingira ya biashara Tanzania. Mchambuzi wa ripoti hiyo ni Bw.David Irwin, ambaye ni mtaalamu wa masuala ya uchumi.

Mchambuzi wa ripoti hiyo Bw.David Irwin alisema kwenye ripoti hiyo biashara ya utalii inatambua kuwa wakati wote kuna umuhimu wa kulipa kodi.

Hata hivyo wahojiwa wengi kwenye utafiti huu wanaona kuwa kupungua kwa mzigo wa mlolongo wa urasimu ungeisaidia skela hiyo vizuri zaidi.

Alisema pia kuwa wafanyabiashara walipendekeza kuwepo kwa mfumo mmoja wa kusaidia serikali kupata mapato kutoka kwenye sekta hii na wakati huohuo kuweka mfumo madhubuti ambao utapunguza gharama ya kufanya biashara na kuwapatia wafanyakazi muda wa kujihusisha na kazi zinazohusiana na biashara yao, kama vile kutafuta masoko, kutoa mafunzo na kujenga uhusiano na wateja.

Bw. Irwin anawanukuu wafanyabiashara ya utalii wakielezea kuwa urasimu usio wa lazima unaleta matatizo kwenye biashara, na kusisitiza kuwa wafanyabiashara wanatambua kuwa serikali inahitaji kukusanya mapato.

Ripoti hiyo ya mtazamo wa wafanyabiashara iliandaliwa ili kutoa vidokezo vya vipaumbele vya kufanyiwa kazi kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanya biashara Tanzania.

Utafiti wa mitazamo ya wadau wa biashara na mazingira ya uwekezaji Tanzania uliofanyika 2011, ulibainisha maoni ya wadau hao kuhusu mazingira ya uwekezaji Tanzania.

## VETA washindi wa pili kimataifa Sabasaba

Na Gladness Mboma

MKATABA



## Vodacom wapunguza gharama za Intaneti

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya Mawasiliano ya Vodacom Tanzania jana imepunguza gharama za huduma ya Blackberry Intaneti kwa wateja wake wa malipo ya kabla

Gharama hizo mpya kwa huduma ya Blackberry Intaneti zitaongeza matumizi ya huduma hiyo, hasa kwa vijana ambao kwa asilimia kubwa hutumia intaneti kwa shughuli mbalimbali kama kupata taarifa na huduma nyingine.

Kwa wateja wa malipo ya kabla, kifurushi cha wiki moja watawezakupata huduma hiyo kwa sh. 7,000 kutoka sh. 20,000, Intaneti kwa sh. 20,000 kwa mwezi ikiwa ni punguzo la kutoka sh. 30,000

Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Bw.Rene Meza, alisema kuwa, gharama hizo mpya zitawasaidia wateja wa Vodocom na pia zitawawezesha kupata kwa urahisi huduma hiyo